# ROHO MTAKATIFU

**Utangulizi**

Kusudi la kijitabu hiki ni kuelezea Roho Mtakatifu ni nani na kazi yake ni gani katika maisha yetu. Pia kitatuonyesha vile tunavyoweza kumpokea Roho Mtakatifu na jinsi anavyojidhihirisha.

Yesu alisema,” *Nami nawaambia,ombeni nanyi mtapewa,tafuteni nanyi mtaona,bisheni nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona, naye abishaye hufunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba , ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai atampa nge? Basi ikiwa nyinyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, Je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho mtakatifu hao waombao”*. (Luka 11:9-13).
Yesu pia akasema, “*Mtu akipenda, atalishika neno langu, na baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake”*, (Yohana 14:23) (Tazama Yohana 14:20-21) Wakati tunapompokea Yesu kama Bwana na mwokozi, Yesu na Baba huja ndani yetu. Hata hivyo Roho Mtakatifu haji kwetu kikamilifu katika roho zetu mpya wakati huu . Lakini elewa kuwa Baba atampatia Roho Mtakatifu yeyote aombaye. Kumpokea Roho Mtakatifu, Luka 11:13

Roho mtakatifu ni nani? Yeye ni Mungu. Yeye ni sehemu ya utatu wa Mungu unaoshirikisha Baba,Mwana(Yesu) na Roho Mtakatifu

Kazi ya Roho Mtakatifu Katika Maisha Yetu

1. Yeye atatufundisha na kutufanya kufahamu neno la Mungu na kutukumbusha yote ambayo Bwana ametuambia. (Yohana 14:26 na Yohana 2:27)
2. Yeye ni msaidizi, ndiye Roho wa kweli (Yohana 14:16-17) aliyetumwa na Baba ulimwenguni wakati wa pentekoste.
3. Yeye hutupa nguvu na ushujaa wa kuwa mashahidi wa Yesu Kristo. (Matendo ya Mitume 1:8)
4. Yesu huhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki na kwamba shetani amehukumiwa na kushindwa.(Yohana 16:8-11)
5. Roho mtakatifu humtukuza na humsifu Yesu na hutufunulia yaliyo ya Mungu. (Yohana 16:13-15, 1 wakorintho 2:9-16)
6. Yeye hutoa karama ili kuhudumia kanisa (1 Wakorintho 12:1-11)
7. Anatuumbia imani ndani yetu tunapolisikia neno la Mungu. Tunapojazwa Roho Mtakatifu maisha yetu katika sifa huinuka.
8. Yeye hutupa nguvu za kuwa na uzima tele tunaopewa na Yesu.

**Atawabatiza kwa Roho Mtakatifu.**

Roho Mtakatifu hayumo ndani yetu wakati tunapompokea Yesu wala hatujii wakati tunapobatizwa. Usiogaope iwapo ulifundishwa kinyume. Tutaliangalia neno la Mungu ili tuweze kuona ni wakati gani anapokuja katika maisha yetu na tujifunze jinsi ya kumpokea.

Yesu alisema......”*Bali ngojeni ahadi ya Baba ambayo mlisikia habari zake kwangu;ya kwamba Yohana alibatizwa kwa maji,bali nyinyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache*”.(Matendo ya Mitume 1:4-5)

Wanafunzi walibatizwa katika jina la Yesu. Walimkiri Yesu kama Bwana wao na wakaamini kuwa alifufuka kutoka wafu. Waliokoka. Lazima wangengoja ahadi ya Baba(Roho Mtakatifu) atumwe kwao. Hawakuwa na Roho Mtakatifu.Yohana mbatizaji alisema haya kumhusu Yesu,"*Mimi nawabatiza kwa maji, bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu*".(Mariko 1:8)

Katika Pentekoste,Roho Mtakatifu alikuja katika ulimwengu na kuwashukia wanafunzi walio kuwa wa kingoja kumpokea kulingana na maagizo ya Yesu na ahadi yake. Sisi hatupaswi kungoja sasa kwa sababu Roho Mtakatifu tayari yumo ulimwenguni na anapatikana kwa wale wote wenye shauku ya kumpokea.

"*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwa wote pahali pamoja. Kukaja ghafula kutoka mbinugni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu,waakanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka*" (Matendo ya Mitume 2:1-4)

Hivi ndivyo neno la Mungu linasema kulifanyika walipojazwa Roho Mtakatifu. Walisema kwa lugha nyingine.

## FILIPO NA KANISA LA KWANZA

"*Filipo akateremka akaingia mji wa Samaria, akawahubiria Kristo na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo. Walipoyasikia na kuona ishara alizokuwa akizifanya. Kwa maana pepo wachafu wakatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu, na watu wengi waliopooza na viwete, wakaponywa. Ikawa furaha kubwa katika mji ule.........Lakini walipomwamini Filipo akizihubiri habari hizo njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo wakabatizwa wanaume na wanawake".* (Matendo ya mitume 8:5-8,12)

Filipo alikuja na kulihubiri neno la Mungu. Watu wakalipokea, wakamkiri Yesu kama Bwana na kuamini katika mioyo yao kuwa Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Waliokoka na kuzaliwa tena. Walibatizwa kwa maji, wakizikwa pamoja na Kristo katika ubatizo. (Warumi 6:3-4)

"*Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu".* (Matendo ya Mitume 2:38)

Neno halisemi tunapompokea Roho Mtakatifu katika ubatizo kama wengi wetu tulivyofunzwa. Neno la Mungu halisemi kuwa Roho Mtakatifu hutujia wakati tunapobatizwa lakini lasema kuwa tutampokea Roho Mtakatifu.

Watu wa Samaria waliokoka- wakazaliwa tena . Lazima wangempokea Yesu katika mioyo yao, na kukiri Yesu ni Bwana na kubatizwa, wakimwamini Bwana Yesu Kristo. Hata hivyo wao hawakumpokea Roho mtakatifu katika kiwango kile. (Tufahamu hivi vizuri)

"*Na mitume waliokuweko Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikumbali neno la Mungu , wakapelekea Petro na Yohana ; ambao waliposhuka, wakawaombea wapokee Roho Mtakatifu, kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao,ila wamebatizwa tu kwa jina lake*

*Bwana Yesu ndipo wakaweka mikono yao juu yao nao wakampokea Roho Mtakatifu"*.(Matendo ya mitume 8:14-17)

Mitume waliwaombea watu hawa ili kumpokea Roho Mtakatifu. Hatujazwi kwa Roho Mtakatifu katika ubatizo wetu kwa maana watu hawa hawakushukiwa na Roho Mtakatifu hata ikiwa walikuwa wameokoka na kubatizwa katika jina la Yesu.

## KUOMBA NA KUPATA

Basi ikiwa nyinyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, Je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?

Tunatakiwa kumpokea Roho Mtakatifu jinsi tulivyompokea Yesu kama Bwana na mwokozi wetu. Tunamwomba Baba atujaze kwa Roho Mtakatifu ili tuweze

i. Kuwa na nguvu za kudumu za Bwana ndani yetu
ii. Tuwe na nguvu za kushuhudia
iii. Kuwaweka wagonjwa mikono nao wapate afya
iv. Kutoa pepo katika jina la Yesu.
v. Kuongea kwa lugha nyingine (Mariko 16:15-18)

Tunatakiwa kujazwa Roho Mtakatifu ili tuweze kutimiza kazi ambayo Yesu Kristo alitupatia ya kulieneza neno lake. Tunatakiwa kumwomba Baba atujaze Roho Mtakatifu kabla ya kujazwa. "Kwa maana bado hajawashukia(Roho Mtakatifu) hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Yesu. (Matendo ya mitume 8:16). Walikuwa wamebatizwa lakini bado hawajashukiwa na nguvu za Roho Mtakatifu . Hii ndio sababu waaminio wengi hawana ushindi katika maisha yao ndani ya Kristo. Wameokoka lakini hawana nguvu katika maisha yao kwa sababu hawana Roho Mtakatifu.

"*Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.*" (Matendo ya Mitume 8:17)

**Kunena kwa lugha nyingine ni dhihirisho**

Haisemekani kwamba watu walipokea lugha ya maombi au ndimi wakati walijazwa Roho Mtakatifu. Hata hivyo, katika maandishi ya Baba zetu wa kanisa la kwanza ni dhahiri kuwa walinena kwa lugha nyingine walipojazwa roho Mtakatifu. Walimpokea Roho Mtakatifu walipokea pia lugha nyingine na ushujaa wa kushuhudia.

Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, "*Nipeni na mimi uwezo huu , ili kila mtu nitakayemwekea mikono yangu apokee Roho Mtakatifu.*"(Matendo ya mitume 8:18-19)

Lazima kulikuwa na dhihirisho wazi ambayo Simoni aliona au alisikia ili kuonyesha kuwa watu hawa walikwisha mpokea Roho Mtakatifu wakati mitume waliwawekea mikono.

"*Petro alipokuwa akiyasema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na petro, kwa*

*sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha na kumwadhimisha Mungu ndipo Petro akamjimbu ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?. Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo.Ndipo wakamshihi zaidi kukaa siku kadha wa kadha."(* Matendo ya Mitume 10:44-48*).*

Wakati watu waliokuwa katika nyumba ya Kornelio walijazwa Roho Mtakatifu, wote walisema kwa lugha nyingine na kumwadhimisha Mungu.Tanbihi. Kujazwa Roho Mtakatifu hakukufanyika wakati watu hawa walibatizwa. Katika hali hii kujazwa kulifanyika baada ya watu hawa kulipokea neno na pia kabla yao kubatizwa . Wayahudi nao walijua kuwa Roho Mtakatifu na uzima katika Yesu ni wa watu wa mataifa pia.

*"Ikawa Apolo alipokuwa Korintho,Paulo, akiisha kupitia kati ya nchi za juu, akafika Efeso, akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; akawuliza, Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. Akawauliza, basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema kwa ubatizo wa Yohana. Paulo akasema, Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akawaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani Yesu. Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu, na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri."*(Matendo ya mitume 19:1-6)

Paulo aliweza kujua kuwa watu hawa waliamini na walikuwa wameokoka. Hata hivyo aliwauliza, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" wakamjibu, "Hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia". Watu wengi leo wamesikia kuhusu Roho Mtakatifu au wanajuamengi kumhusu, lakini hawajui jinsi anvyokuja au kusudi lake na kazi yake katika maisha ya wanoamini. Wamesikia kuhusu wokovu.wanajua wameokoka kwa msingi wa neno la Mungu katika Yesu Kristo. Hata hivyo hawajawahi kusikia kuhusu utele wa Mungu walioupata katika Roho Mtakatifu. Hii ndiyo hali ilikuwepo pale Efeso.

Watu walibatizwa katika jina la Yesu . Paulo akaweka mikono yake juu yao ili wampokee Roho Mtakatifu. Walimpokea na kunena kwa lugha nyingine.

*"Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani, akamwekea mikono akisema, "Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu yeye aliyekutokea katika njia uliyoijia, upate kuona tena. Ukajazwa Roho Mtakatifu. Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba , akapata kuona, akasimama, akabatizwa."* (Matenda ya Mitume 9:17-18)

Paulo alipatahuduma yake kutoka kwa Bwana alimpokea Roho mtakatifu. Sisi sote tuna huduma kutoka kwa Bwana . Hata hivyo hatutakuwa na nguvu za kuiendesha huduma hiyo mpaka tujazwe kwa Roho Mtakatifu.

"*Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya nyote.*" (1 Wakorintho 14:18).
Paulo ansema kuwa wakati alipojazwa Roho Mtakatifu alipowekewa mikono na Anania, alinena kwa lugha nyingine. Kunena kwa lugha nyingine humpata kila anayempokea Roho Mtakatifu.

**Kunafanyikaje wakati tunaomba kwa Roho Mtakatifu**

(1) Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali hunena na Mungu, maana hakuna

asikiaye , lakini ananena mambo ya siri katika roho yake. (1 Wakorintho 14:2)

(2) Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. (1 Wakorintho 14:14)
(3) Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu (kupitia kwa Roho Mtakatifu aliye ndani yangu) huomba lakini akili zangu hazina matunda- hazizai matunda na hazimsaidii yeyote. (1 Wakorintho 14:4)
(4) Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake....” (1 Wakorintho 14:4)

(5) Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, Lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo alijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu. (Warumi 8:26-27)
(6) Bali nyinyi, wapenzi , mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu. (Yuda 20)

Baada ya kupokea kujazwa Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu huishi ndani yetu. Wakati tunaomba kwa lugha , tunaomba moja kwa moja kwa Mungu kutoka kwa roho zetu mpya, tukiongozwa na Roho mtakatifu. Kwa kuwa akili zetu (Zinazozaa mashaka woga, hofu n.k) zimepitwa, basi tunaomba kwa sifa zifaazo na maombi yafaayo kwa Baba yetu kutoka roho zetu mpya zisizoharibika. (1 Petro 1:23)

Tukiwa katika hali ambapo twaweza kuwa hatujui jinsi tunavyotakiwa kuomba, Roho Mtakatifu hutuombea tunapoomba katika Roho au lugha kwa maana Roho Mtakatifu hawezi kuugua, sisi ndio huugua kama vile Roho Mtakatifu anavyotuongoza katika roho zetu mpya na tunanena au kuugua yote tunayopewa naye kulingana na mapenzi ya Mungu kwetu. Hivi ndivyo, “*Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wampendao katika kuwapia mema, yaani wale walioitwa kwa jina lake.”* (Warumi 8:28)

Tunaponena kwa lugha Mungu husema kwamba tunajijenga na kujiboresha. Tunajenga imani yetu iliyo takatifu sana. Maisha yetu ya sifa ndani ya Mungu huhuishwa. Kuomba katika lugha kunalinganishwa na kuweka betri moto kunatufanya “Kuwa moto ” katika Roho Mtakatifu. Wakati unapofika wa nguvu za Mungu kutembea katika maisha yetu, nguvu zitakuwepo.

JINSI YA KUPOKEA

Mimi binafsi nilikuwa na maswali mengi kuhusu Roho Mtakatifu na lugha nilikuwa nimefundishwa kuwa nilimpokea Roho Mtakatifu wakati nilibatizwa. Hata hivyo, nilipotafakari neno la Mungu, nilipata kuwa Yesu alisema tumuombe Baba ili tujazwe Roho Mtakatifu ( Luka 11:13) kwa hivyo, katika kulitii neno la Mungu nilimomba Baba anijaze. Nilijazwa Roho Mtakatifu kwa misingi ya neno la Mungu na ahadi (Luka 11:13) “*Ombeni nanyi mtapetwa*” (Luka 11:9) *“Yoyote myaombao mkisali amini yakwamba mnayapoke, nayo yatakuwa yenu*” (Mariko 11:24)
Nilijuwa kuwa nilijazwa Roho Mtakatifu. Hata hivyo, sikujuwa wala kufunzwa wakati hua kuwa ningenena kwa lugha na si kunena kwa lugha wakati hua sio kwamba singeweza lakini sikujuwa kuwa Mungu tayari amenipa lugha hii mpya wakiti nilipokea Roho Mtakatifu.

Nilipokea lugha mpya au lugha ya kuomba wakati nilipokea Roho Mtakatifu lakini sikujua jinsi ya kuinena. Hakuna aliyeniambia nifungue kinywa changu na kiunena kinywa changu kilikaa kikiwa kimefungwa nikingoja mbingu zifunguke ghafla ili ninene kwa lugha nyingine jinsi neno la Mungu

linavyosema.

Niliamini kwa muda mrefu kuwa Mungu hakunipatia lugha hii au lugha ya maombi (jambo ambalo si kweli lakini nililowaza katika kutojua kwangu) Niliamini kuwa Mungu alifikiria kuwa siihitaji.

Nilitembea katika kiburi cha kiroho na kutojua mpaka siku moja nikaanza kuongozwa kutoka ndani mwangu kuwa na ushirika wa ndani zaidi na Mungu katika sifa. Nilianza kulisoma neno la Mungu na kuwatafuta waliomsifu Mungu kweli. Nilitafuta mahali ambapo ushindi wa nguvu za Mungu ulitembea.

Nilifikiria kuwa Roho Mtakatifu angeuchukua ulimi wangu na kuufanya unene katika lugha ya maombi. Lakini Roho hawezi kunifanyia hivyo. Nilingudua kuwa ulimi wangu ndio hunena ukiongozwa na Roho Mtakatifu.

Kuna wengi wanaoamini Yesu Kristo, wazuri pia ambao huamini kimakosa kuwa lugha au lugha ya maombi si ya kila anayeamini na ambaye amejazwa Roho Mtakatifu. Nilikuwa nikiamini hivi kwa kutojua kwangu. Wengine hawaamini lugha na karama za Roho ni za sasa. Je kufufuka ni kwa sasa ?.
Ikiwa Yesu ni yule yule jana leo na milele-ikiwa neno lake hilitaondoka- hivi ndivyo ahadi zake na Roho Mtakatifu katika Agano Jipya zinavyofanya leo kama zilivyokuwa wakati ule. Hatuwezi kuamini sehemu fulani tu za neno la Mungu na kuacha zingine. Kazi za Mungu katika Roho Mtakatifu hazijabadilika kwa kanisa lake na hazitaondolewa mpaka Kristo arudi.

**Tofauti kati ya lugha ya maombi na karama za kazi ya huduma**
Nilifurahia sana wale walipokea lugha mpya lakini nilikuwa nikiamini kwamba haikuwa ya watu wote. Ningenukuu, *"Na Mungu ameweka wengi katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wangojwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha. Je, wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? Wote wana karama za kuponya wangojwa? Wote wananena kwa lugha? Wote wafasiri?(1 Wakorintho 12:28-30)*

Ni kweli kuwa si sisi sote tutakaohudumia mwili wa Kristo kupitia karama hizi. Vile tutakavyohudumu kutategemea Roho Mtakatifu. Hata hivyo Bwana alinionyesha kuna tofauti kati ya karama za kazi ya huduma na lugha au lugha ya maombi inayowajia wote waliojazwa Roho matakatifu. Kwa nini lugha au lugha ya maombi hunufaisha tu anayeitumia wala si kanisa (1 wakorintho 14:4) Karama ya kazi ya huduma ya kunena kwa lugha na kutafsiri husaidia watu wote.

Siku moja nilipokuwa nikitafakari juu ya karama za Roho . Bwana alinifunulia haya,'*Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa apendavyo Roho yeye yule na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja*.(Wakorintho12:8-9)Niliuliza Bwana 'Jambo hili linahusianaje nawe kunipa Roho au kutonipa?'Mungu alinionyesha kuwa amenipa mimi na wote waaminio kiasi cha imani kumpokea Yesu na kuokolewa. (Warumi 12:3) Lazima tuwe na imani ili tuokolewe na kumfurahisha Mungu. (Waefeso 2:8-9, Waebrania 11:6) lakini nikasoma kuwa Roho Mtakatifu huwapa imani wengine. (1 Wakorintho 12:9) karama hii ya imani ni kipawa cha kipekee kilicho juu na kupita imani ambayo sisi sote tunayo kazi ya huduma ya Mungu iweze kutimizwa nami nikafahamu.

Kwa njia hiyo hiyo Mungu amenipa lugha au lugha ya maombi na waaminio wote ambao wamepokea Roho Mtakatifu, hata hivyo hii si karama ya huduma ya aina ya lugha kama ilivyotajwa katika (1Wakorintho 12:28-30) ambayo si kila anayeamini hupatiwa na Roho Mtakatifu. Katika Matendo ya Mitume wote waliompokea Roho Mtakatifu walinena kwa lugha nyingine. Niliwekwa huru kuamini katika lugha mpya wakati nilipokea Roho Mtakatifu(kama ilivyofanyika katika kitabu chaMatendo ya Mitume) kutoka wakati huo nilipata pia (katika kutii neno la Mungu) kuwa kila anayezaliwa tena, tunapomwekea mikono juu yake ili ampokee Roho Mtakatifu pia hupokea lugha mpya ili kumwadhimisha Mungu na kumsifu Mungu na kuijenga imani take iliyo takatifu sana. (Yuda 20)
Kuomba katika lugha (au Roho Mtakatifu) kunawasha imani ambayo tumepewa na mungu kwa misingi ya neno lake. Kuomba katika lugha hakutuongezei imaniMungu na kuomba kwa lugha Mungu hutuwezesha kupigana vita na kutupa ushindi.

## KUTUPA NGUVU

Wakati watu katika Matendo ya Mitume walijazwa Roho Mtakatifu walikuwa na“moto” Hakuna angezuia ushuhuda wao kuhusu Bwana Yesu Kristo kuendelea mbele . Hata ikiwa walipata mateso kwa kumshuhudia Yesu Kristo, ujasiri wao haungevia. Moto wa Roho Mtakatifu ulichoma ndani yao.
Walifurahi na kusifu Bwana hata walipokuwa wakitupiwa simba na walikuwa na amani, furaha na upendo.

Hakika wao walikuwa na kitu kilichowachochea. Watu kwa kweli hawana nguvu kama hizo wakiwa peke yao. Walikuwa na Roho Mtakatifu-Msaidizi aliyetumwa kutoka kwa Baba. Hata tuwe katika hali gani, Mungu atatupatia ushindi kwa utukufu wake. Wengine watashindwa kwa nini mimi na wewe tunamfurahia Yesu. Tunaweza kuwa na “moto” wa mungu, Roho Mtakatifu akitupa nguvu katika maisha yetu kwa ushindi.

Ili kupata wokovu, tinatakiwa kutubu, kumwamini Yesu(warumi 10:9-10) na kubatizwa(Matendo ya Mitume 2:38). Ili tuweze kupata nguvu za Mungu tunatakiwa kujazwa kwa Roho Mtakatifu, aliye mfariji. Hii ndiyo sababu iliyowafanya mitume kuwauliza watu,”Mlipokea Roho Mtakatifu?” Mungu anataka kutupa zawadi yake , nguvu za Mungu ili huduma yake idhihirike ndani yetu na tuweze kuwafikia wengine.
“*Naye Yesu akawaambia, enendeni ulimwengu wote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Ni ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa jina langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watashika nyoka, hata wakinywa kitu cha kufisha hakitawadhuru kabisa, wataweka mikono yao juu ya wangonjwa, nao watapata afya.......... Nao wale (wanafunzi) wakatoka, wakahubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulidhibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo*. Amina”
(Mariko 16:15-18,20). Katika nguvu za jina la Yesu ishara hizi zitafuata wote waaminio. Karama za Roho katika 1Wakorintho12 zitaanza kufanya kazi katika maisha yetu jinsi Roho Mtakatifu anavyotuelezea.

*“Lakini mtapokea nguvu, akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu......... na hata mwisho wa nchi*” (Matendo ya Mitume 1:8)

Tumeokoka na kupata nguvu kupitia kwa Roho Mtakatifu, sio tu kupokea aina ya baraka kutoka kwa Mungu, bali pia tuwe na ujasiri katika huduma ambayo Bwana amempa kila mmoja wetu. Tunatakiwa kumshirikisha Yesu Kristo, neno lake na jinsi anavyomaanisha katika maisha yetu kwa wengine.

Wakati mmoja katika mkutano, Bwana alinena, "Watu wangu wanatamani kufanana nami. Wanatamani kuwa na upendo,wema wenye furaha, wenye amani, wasamehevu n.k. Hata hivyo, ikiwa watu wangu hakika watafanana nami katika kila kitu, basi lazima waenende akitaka karama zote za Roho Mtakatifu jinsi nilivyofanya.

Tunda la Roho ni la utakatifu wa maisha . Yanatujia pamoja na kuzaliwa upya ndani ya Yesu na kutenda sawa na neno la Mungu.Karama za Roho Mtakatifu ni za huduma na nguvu katika kushuhudia ambazo huja kwa kujazwa Roho Mtakatifu.

Sababu za kunena kwa lugha.

1.Ni dhihirisho la kujazwa Roho Mtakatifu(Matendo ya Mitume 2:4,10:46)
2.Ni ukumbusho wa kila wakati wa uwepo wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu(Yohana 14:16-17)
3.Kujijenga kupitia mawasiliano ya kiungu naMungu (1 wakorintho 14:2,4:14)
4.Kuipa imani yetu nguvu(Yuda 20)
5.Kuombea yanayojulikana na yasiyojulikana na mapenzi ya Mungu.(Warumi 8:26-28)
6.Hutuwezesha kuufuga ulimi wetu. Kutuondolea au kuzuia ya ulimwengu kututawala wakati roho zetu zinaomba Mungu.(1Wakorintho 14:2, Yakobo 3:1-8)
7.Kumshukuru Mungu na kumwabudu katika Roho.(1 wakorintho 14:15-17, Yohana 3:1-8)
8.Hutupa pumziko na raha(Isaiya 28:11-12)
9.Hutuwezesha kupigana vita vya kiroho, hutusaidia katika uombezi na hufungua karama zingine za Roho.(Waefeso 6:18, Warumi 8:26-28), 1 wakorintho 14:2)
10.Huinua umakinifu wa mwongozo wa Roho Mtakatifu. (Warumi 8:14, 26-28)

## OMBI LA KUMPOKEA ROHO MTAKATIFU

Baba katika jina la Yesu,
Namkiri Yesu kama Bwana na mwokozi wangu.
Naamini katika moyo wangu kuwa Yesu alifufuka kutoka wafu.
Naamini kuwa Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu-nakushukuru kuwa umenifanya mtoto wa Mungu.
Namkataa shetani na njia zake zote.
Na kulingana na neno lako na ahadi kuwa ikiwa nitaomba
kumpokea Roho Mtakatifu wako, utanipatia Roho Mtakatifu wako na nitanena kwa lugha nyingine.(Luka 11:13)
Nakuomba unipatie Roho Mtakatifu wako na lugha mpya.
Nakushukuru kwa kunipatia Roho Mtakatifu na nakushukuru
kuwa sasa nasema kwa lugha nyingine nikikusifu.
Katika jina la Yesu .Amina.

**Maagizo Zaidi**

Ikiwa umeomba kupokea kwa misingi ya neno la Mungu na ahadi sasa umejazwa Roho Mtakatifu na utanena kwa lugha nyingine. Usiongee kingereza  au lugha yako uanyoitumia. Anza kutoa sauti kwa ulimi wako naye Roho Mtakatifu ataanza kuzifanya sauti hizo maneno ya lugha yako mpya. Haitakuwa kama chochote akili yako imewahi kusikia, kwa hivyo usiiache akili yako ifikirie ni upuuzi. Ni baraka kutoka kwa Mungu.  Usiyafanye maneno kwenye akili yako kwa maana huombi kwa akili zako bali ni kutoka kwa roho yako mpya. Tazama Yesu. Sifu Mungu endelea kunena. Endelea kutumia lugha yako ya maombi kila siku. Inaweza kuanza pole pole lakini itaongezeka unapolendelea kuitumia.sasa unaweza kumwabudu Mungu katika Roho na kweli.

© 1987, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,
all rights reserved,

www.glorytogod.org